TANGAZO LA SERIKALI Na. 311 la tarehe 28/4/2023

SHERIA YA MIPANGOMIJI
(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA ENEO LA ZIWANI - NYARUGUSU YA MWAKA 2023

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kurasimisha Makazi Yasiyopangwa Eneo la Ziwani - Nyarugusu ya mwaka 2023.

Utangazaji wa eneo la upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji la mpango wa urasimishaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipangomiji.

Mpangokina wa eneo

3. Mipangokina ya eneo lililoainishwa katika Jedwali inaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Geita.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la urasimishaji lipo ndani ya mipaka ifuatavyo-

"Mpaka unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba A yenye majira - nukta 414614MS, 9656287KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki katika uelekeo wa KZ161°MS kwa umbali wa kilomita 1.02 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba B yenye majira - nukta 416092MS, 9658166KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki katika uelekeo wa 114° kwa umbali wa kilomita 0.6 hadi kwenye alama ya mpaka ya upiamji namba C yenye majira - nukta 417046MS, 9658266KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Magharibi katika uelekeo wa 120° kwa umbali wa kilomita 0.6 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba D yenye majira - nukta 417742MS, 9657285KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi katika uelekeo wa 132° kwa umbali wa kilomita 0.3 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba E yenye majira - nukta 385787MS, 9671766KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Magharibi katika uelekeo wa 87° kwa umbali wa kilomita 0.9 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba F yenye majira - nukta 415969MS, 9655237KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini - Mashariki katika uelekeo wa 103° kwa umbali wa kilomita 1 hadi ulipoanzia"

Dodoma,
17 Machi, 2023

ANGELINE S. MABULA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*